JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Simu: +255 26 2322761-5
Nukushi: +255 26 2324218
Barua Pepe: cna@bunge.go.tz

BUNGE LA TANZANIA

Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S.L.P 941,
40490 Tambukareli,
DODOMA

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Mkutano wa Nne wa Bunge umeanza leo tarehe 26 Agosti, 2026 na utamalizika tarehe 04 Septemba, 2026 Jijini Dodoma.

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika Mkutano huu ni pamoja na **Maswali ya Wabunge ambapo takribani ya Maswali ya Kawaida 140** yataulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali.

Aidha, katika kipindi cha **Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu, wastani wa Maswali 16 yanatarajiwa kuulizwa** na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Shughuli nyingine zitakazofanyika ni kama ifuatavyo:-

**a) Miswada ya Sheria**

Jumla ya Miswada mitano (5) ya sheria iliyosomwa kwa Mara ya Kwanza katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu itawasilishwa kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa. Miswada hiyo ni ifuatayo:-

i. **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026;**

ii. **Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026;**

iii. **Muswada wa Sheria ya Mikopo kwa Dhamana za Mali zinazohamishika wa Mwaka 2026;**

iv. **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026 na**

v. **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2026.**

**b) Azimio la Bunge**
Katika Mkutano huu, Serikali inatarajia kuwasilisha Azimio moja ili Bunge liridhie. Azimio hilo ni kuhusu Mapendekezo ya Kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa Taasisi ya Ukuzaji Maendeleo ya Kijani Duniani.

**c) Taarifa ya Kamati**
Vilevile Bunge litapokea Taarifa ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Pili na Mkutano wa Tatu wa Bunge.

Ratiba yote ya Mkutano wa Bunge inapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni ***www.bunge.go.tz.***

**Imetolewa na:** Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma,
Ofisi ya Bunge,
**DODOMA.**

**26 Agosti, 2026**